# MAPITIO YA KITABU

JINA: **Misingi ya Hadithi Fupi (kurasa 219)**
MTUNZI: Mbunda Msokile
MCHAPISHAJI: DUP (1992)
MPITIAJI: J.S. Madumulla

## 1.0 Utangulizi

Mbunda Msokile si jina geni katika dunia ya waandishi wa hadithi na wahikiki wa fasihi. Yeye ni mwandishi anayejulikana, hususan wa hadithi fupi za kisasa. Hadithi zake kadhaa zimejitokeza katika magazeti, kama vile MZALENDO na KIONGOZI. Hadithi nyingine zimo katika diwani yake ya **Nitakuja kwa Siri (1981)**. Amepata kuandika pia hadithi ndefu (au riwaya) ambazo baadhi yake ni **Usiku Utakapokwisha** (1990), **Thamani ya Ukubwa** (1979) na **Dhihaka ya Mume** (1979). Aidha, Mbunda msokile ni mhakiki ambaye ametoa mchango mkubwa katika kuliendeleza somo la Fasihi ya Kiswahili (Sekondari na Vyuo) kupitia gazeti la **Kiongozi.** Akishirikiana na wataalam wengine aliandika kitabu cha uhakiki kiitwacho **Uhakiki wa Vitabu vya Fasihi** (1990). Kitabu chake kingine, **Misingi ya Uhakiki wa Fasihi** kilichapishwa na Heinemann Kenya (1992). Hali kadhalika, katika uga huo wa uhakiki, alitoa mfululizo wa viongozi vya uchambuzi wa ushairi, riwaya na tamthilia za Kiswahili. Baadhi yake ni **Uchambuzi na Uhakiki: Harusi, Uchambuzi na Uhakiki:Lina Ubani, Uchambuzi na Uhakiki: Fungate ya Uhuru**, n.k. Mfululizo huo unaitwa "Miongozo ya Lugha na Fasihi".

**Misingi ya Hadithi Fupi** ni kitabu kingine cha mwandishi huyu ambacho, kwa namna moja au nyingine, kinathibitisha kuwa hakika alikuwa ni gwiji wa uandishi wa hadithi fupi, kwani alizijua kunga zake vilivyo. Ama, kinamthibitisha kuwa alikuwa ni mtaalam wa uwanja huo kwani alizamia nadharia yake kwa mapana, marefu na kina cha kuridhisha. Uwanja huu wa hadithi fupi - ziwe za kifasihi simulizi au za kisasa - unajulikana sana katika ulimwengu wa Kiswahili, ijapokuwa katika upande wa uhakiki umegusiwagusiwa tu. Mbunda Msokile anaweza kusemekana kuwa ni mtu wa kwanza kukizamia kipengele hiki kwa kina hicho. Lengo la makala hii ni kukipitia kitabu cha **Misingi ya Hadithi Fupi**.

## 2. Muhtasari

Kitabu hiki kina sehemu nne kuu. Ya kwanza ni "Yaliyomo"ambayo pia ina dibaji iliyoandikwa na Prof. Rajmund Ohly na utangulizi wa mwandishi. Ya pili inahusu nadharia ya hadithi fupi na fasihi. Ya tatu ni diwani ya hadithi fupi ambazo zimeandikwa na watunzi maarufu wa hadithi, E. Kezilahabi, M. Mulokozi, J. Rutayisingwa, M. Mohamed na M. Msokile mwenyewe. Ya nne ni nyongeza iliyo na maelezo, bibliografia, istilahi za fasihi na faharisi.

### 2.1 Yaliyomo: Utangulizi wa Prof. Ohly:

Ohly, akitofautisha kati ya hadithi za fasihi-simulizi (ngano) na hadithi fupi za kisasa, anasema kuwa ngano hutegemea **uwezo wa kiutendaji** wa msanii, na kwamba hadithi fupi za

kisasa hutegemea **uwezo wa kisanii**, kiwango cha elimu na ujuzi wa mtunzi kuandika alichonacho. Hadithi fupi za kisasa anazigawa katika mafungu mawili au matatu: za vitabuni (fupi zaidi), za magazetini (fupi kiasi) na za redioni (fupi). Ufupi huo unadhibitiwa na muda, wakati, nafasi, na wepesi wa kueleweka.

Kuhusu uchapishaji wa hadithi fupi, Ohly anadai kuwa lengo la kutunga hadithi fupi, hususan za magazetini, ni kutaka **zitumike haraka**. Hivyo uhai wake unaweza kulinganishwa na ule wa gazeti, ambapo gazeti la siku lisiposomwa siku linayokusudiwa lisomwe, huwa limepitwa na wakati. Hadithi hizo fupi za kisasa aghalabu huendana na maisha halisi.

Kisha Ohly anaelezea maumbo ambayo hadithi fupi za kisasa zinaweza kuwa nayo, k.m. kutumia mbinu za kingano, tarijama, dayologia (mazungumzo), n.k. Hatimaye, Ohly anayaona makusudio mawili katika kitabu cha Mbunda Msokile cha Misingi ya Hadithi Fupi, ambayo ni:

1. Kuwapa waandishi chipukizi kunga za uandishi wa hadithi fupi za kisasa. Amefanya hivyo kwa kutoa nadharia ya uandishi ambayo imefafanuliwa kwa mifano halisi ya hadithi fupi za fasihi-simulizi na za kisasa.

2. Kuwanufaisha wapenzi na wataalam wa fasihi kwa jumla kwa bibliografia na istilahi teule inayojitokeza katika sehemu ya mwisho.

## 2.2 Nadharia ya hadithi fupi na fasihi:

Sehemu hii ina sura tano, na ndiyo inastahili kuitwa uti wa kitabu hiki. Sura ya kwanza inashughulikia maana ya hadithi kwa jumla na ile ya hadithi fupi. Wataalam kadhaa wamerejewa ili kuibainisha maana hiyo, k.m. Esenwein, Finnegan, Scholes na Kellogg, Muhando na Balisidya, Mphahlele, Senkoro, Ohly n.k. Katika sura hii mtunzi ameweka wazi tofauti zilizopo baina ya ngano na hadithi fupi za kisasa:

| Ngano | Hadithi fupi za kisasa |
|---|---|
| 1. muundo rahisi/sahili | - muundo mgumu kiasi |
| 2. tuko (episode) moja | - tuko moja au zaidi, lakini si mengi |
| 3. mandhari si halisi | - mandhari halisi |
| 4. wakati hauna mpaka (hivyo si halisi) | - wakati halisi (una mpaka) |
| 5. ni fupi | - ndefu kiasi |
| 6. wahusika bapa (vielelezo) | - wahusika halisi (si vielelezo) |
| 7. wahusika hawana majina halisi (mf. mtu na mkewe; mfalme, nokoa, n.k.) | - wana majina halisi |
| 8. mhusika mkuu mmoja, tena muhimu sana | - si lazima awe mmoja; si lazima awe muhimu sana |
| 9. mwanzo na mwisho maalum | - ni maalum |

Katika sura hii pia kuna dai kwamba ngano si za kubuniwa, isipokuwa hadithi fupi za kisasa. Ni hoja ambayo imejitokeza kwa namna fulani pia katika utangulizi wa Ohly. Akiihitimisha sura ya kwanza, mtunzi anaziorodhesha sifa au kaida za hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili hivi: iwe na kadhia moja, mhusika mmoja au wawili, masimulizi ya kubuni, **lakini yasiwe uongo**, maisha yaliyosanifiwa, iwe na msuko, mawanda yasiwe mapana na kusiwe na mchangamano wa masimulizi.

Sura ya pili inahusu itikadi na uandishi wa hadithi ambapo mtunzi anasisitiza kuwa kila kazi ya fasihi inahusiana na itikadi fulani, na hivyo ni muhimu kwa mtunzi yeyote kujijua nafasi na wajibu wake, atambue kazi yake ina mdhamini gani, huku akijali mipaka na athari za udhamini huo. Ni muhimu kutambua mipaka ya uhuru wa mwandishi pia.

Sura ya tatu inahusu fani na maudhui ambapo mtunzi anadai kuwa **tawi** ni kisawe cha **utanzu**, na **fani** ni kisawe cha **umbo**. Pia anakubaliana na wale wanaodahili kuwa fani na maudhui ni vitu visivyotenganishika (mf. Nkwera, Kiango na Sengo, Muhando na Balisidya, n.k.).

Sura ya nne imeishughulikia fani. Vipengele vilivyoshughulikiwa ni wahusika (ujenzi wao, aina zao), matumizi ya lugha (methali na misemo, tamathali za usemi, tamathali za mlinganisho, tamathali za msisitizo na aina nyinginezo), matumizi ya ucheshi na ishara, mitindo ya hadithi fupi (ya jazanda, kimaelezo, kimasimulizi, kuhoji, monologia, dayologia), msuko wa matukio (wa kioo, wa kibarua, msago, mwisho-kati-mwanzo, mwanzo-kipeo), **mashairi na nyimbo,** kilele na mpomoko. Vipengele hivi vimeelezwa kwa mifano ambayo inaeleweka vya kutosha.

Sura ya tano imelishughulikia suala la uandishi wa hadithi fupi za Kiswahili. Hapa mtunzi anaijadili dhana ya 'kubuni' na jinsi inavyoendana na hadithi fupi za kisasa. Baada ya hapo baadhi ya mambo yanayohitajika katika ubunaji wa hadithi fupi yametajwa na kuelezwa (k.m. uzoefu, utafiti, fikra, kipawa, sifa, uandishi kwa vidokezo au bila vidokezo) jinsi yanavyoweza kumsaidia mwandishi chipukizi. Kwa hiyo, sura ya tano inaweza kusemekana kuwa ni ya kumfunza mwandishi chipukizi mbinu za uandishi baada ya kuwa amepitishwa katika nadharia iliyomo katika sura zilizotangulia.

### 2.3 Diwani ya hadithi fupi

Kama ilivyogusiwa hapo nyuma, sehemu hii ina hadithi fupi teule zilizoandikwa na watunzi ambao ni miongoni mwa watunzi maarufu wa fasihi ya Kiswahili. Hadithi hizo ni "Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani" na "Wasubiri Kifo" (na E. Kezilahabi), "Siri ya Bwanyenye" (na M. Mulokozi), "Ndumila Kuwili" (na J. Rutayisingwa), "Kijana Yule" (na M. Mohamed), "Nyota ya Chiku", "Kiumbe Mzito" na "Uchungu" (na M. Msokile). Hadithi hizi zina sifa za hadithi fupi za kisasa na zimetumiwa na mtunzi katika sehemu ya nadharia kuthibitisha hoja moja au nyingine inayohusu hadithi fupi.

### 2.4 Nyongeza: Maelezo, Bibliografia, Istilahi na Fahirisi:

Katika sehemu hii ya mwisho, mtunzi ameorodhesha bibliografia na istilahi teule ambavyo vitamsaidia msomaji kupata mwanga zaidi juu ya hadithi fupi na fasihi kwa jumla.

## 3.0 Maoni

### 3.1 Ya jumla:

Kwa jumla, mchango wa M. Msokile katika taaluma ya hadithi fupi ni mkubwa. **Misingi ya Hadithi Fupi** ni kitabu cha kwanza cha kinadharia cha aina yake ambacho kimeandikwa kwa Kiswahili juu ya nadharia na uandishi wa hadithi fupi. Kama ilivyogusiwa hapo nyuma, kinaaridhia nadharia na kunga za hadithi fupi, hususan za (au katika) Kiswahili. Kitabu hiki kinampa nafasi mtu aliye katika mazingira ya darasa la fasihi kuufahamu vema uga huu wa hadithi fupi na kuutofautisha kwa urahisi na matawi au tanzu nyingine za fasihi hususan zile zitumiazo maandishi ya mjazo. Hali kadhalika kitabu kinampa fursa mwanagenzi wa uandishi wa hadithi kujifunza mengi juu ya usanii huo.

## 3.2 Kuhusu Sehemu ya I:

Kwa maoni yetu, kichwa kingekuwa "Nadharia ya Hadithi Fupi" tu, badala ya "Nadharia ya Hadithi Fupi na Fasihi". Neno 'Fasihi' lingeachwa. Sababu ni kwamba sehemu hii inajadili kuhusu nadharia ya hadithi fupi tu, na si fasihi katika mapana yake.

## 3.3 Kuhusu Nadharia ya/za Uandishi wa Hadithi:

### 3.3.1 Sheria/kunga:

Mengi ya yaliyojadiliwa katika kipengele hiki yamefafanuliwa kwa jitihada kubwa na mifano kadhaa. Ni vema kuwa mtunzi anaeleza wazi kuwa "hakuna sheria zilizowekwa ili zifuatwe na kuzingatiwa ili ziandikiwe hadithi fupi" (uk. 95). Kauli hii ni ya msingi. Tofauti na mashairi na tamthilia, uwanja wa hadithi haukudhibitiwa na sheria yoyote. Ni uwanja huria ambao umekuwa na mnyumbuliko (flexibility) wa hali ya juu kama **amoeba**. Kunga ambazo zinajitokeza katika **Misingi ya Hadithi Fupi** juu ya uandishi wa hadithi fupi (uk. 94 - 104) ni mapendekezo tu yanayoonyesha njia mojawapo ya kuweza kuandika hadithi fupi. Si kunga hizo tu ambazo zimependekezwa na wataalam wa fasihi, bali kuna nyingine kadhaa (taz. **Fasihi**, 1983). Kunga hizi, ambazo ni mbalimbali, zinatubainishia kuwa kila mwandishi, hatimaye, ana namna yake ya kuandika, ijapokuwa panaweza kuwa na kufanana fanana na hata kuigana na kuathiriana baina ya waandishi. Hatimaye kuna Sh. Robert mmoja tu kama kulivyo na M. Msokile mmoja tu.

### 3.3.2 Istilahi:

Kuna suala la utata wa istilahi zilizotumika katika kitabu hiki. Mifano ni kama vile tawi na utanzu au fani na umbo. Tukianza na tawi na utanzu, je, hivyo ni visawe? Yaani, ni maneno yenye maana moja? Kwa maoni yetu ni kuwa utanzu ni utagaa. Yaani ni kijitawi cha tawi. Hali kadhalika, kwa maoni yetu, fani inajumlisha umbo la ndani na la nje, yaani inajumlisha maumbo. Kwa jinsi hiyo haitakuwa sahihi kudai kuwa fani ni sawa na umbo. Kwa maneno mengine, kuna haja ya kuifanyia kazi zaidi istilahi ya fasihi ili iwe wazi zaidi kwa msomaji wa nadharia ya fasihi. Kisha kuna vijineno kama vile 'ming'ong'oso', 'vidoko' (uk. 8), n.k. ambavyo vilipaswa vielezwe zaidi dhima zao katika fasihi, na hata kuweza kuingizwa kwenye orodha ya istilahi. Kwa upande wa istilahi kwa jumla mwandishi amejitahidi kuiorodhesha mwishoni. Hata hivyo, baadhi ya maneno yanahitaji masahihisho (mf. mtiririko si 'structure', uk. 205; 'plot' si msuko/msuko-msago, n.k.), na marekebisho mengine ya hapa na pale.

### 3.3.3 Fani na Maudhui:

Kuhusu fani na maudhui, ni kweli havitenganishiki. huenda wataalam waliozungumzia kikombe na chai, chungwa na ganda lake, n.k. walikuwa na maana hiyo hiyo ya kutotenganishika, **kwani katika hali halisi** fani na maudhui havitenganishiki, **kumbe katika nadharia** mambo hayo yanatenganishika. Mwandishi angewakosoa wataalam hao katika msingi huo. Kwa kufuata msingi huo basi, kosa la wataalam hao ni kuwa hawakulijali umbo la ndani la kazi ya sanaa. Kwao kila kitu cha ndani ni maudhui tu. Suala hili halijitokezi wazi katika kitabu hiki. Aidha maudhui yamepewa nafasi ndogo tu ya kujadiliwa ukilinganisha na sehemu kubwa na ndefu iliyopewa fani. Hatimaye, pamoja na ukweli kwamba fani na maudhui havitenganishiki, na kwamba si sahihi kukitukuza mno kimoja kuliko kingine, lakini kimoja hakina budi kuwa cha msingi. Ndiyo maana kuna wataalam wanaodai kwa kutumia misingi ya kiyakinifu kuwa maudhui ndiyo hatimaye huzua na kudhibiti fani. Aghalabu maudhui huja kwanza, na kufuatwa na fani.

### 3.3.4 Ubunifu:

Kisha kuna suala la ubunifu. Mtunzi, akiungwa mkono na Ohly kwa namna fulani, anazitoa ngano kutoka kwenye ubunifu. Mtunzi anaandika, "ngano ni hadithi za simulizi **za mapokeo**, si **za_kubuniwa** wala hazichukui mandhari na mazingira ya kiuhalisia" (uk.7). Sababu kubwa anayoishikilia mtunzi ni kuwa ngano ilikwisha kubuniwa, sasa **inasimuliwa upya**. Aidha, anaongeza kuwa fanani ana uwezo wa "kuingiza vitu vya kubuni ambavyo kwa asili yake havikuwa katika masimulizi ya awali" (uk. 7).

Iwe iwavyo, lakini ukweli ni kwamba ngano, kama ilivyo hadithi yoyote, ni ya kubuni, isipokuwa kama **inasomwa**. Ngano inapopokelewa, aghalabu kinachopokelewa hasa huwa ni kiunzi tu, kazi kubwa huwa kwa fanani kutumia ufundi wake wa **kubuni** ili kukipatia manyama kiunzi hicho. Hali kadhalika, ni sahihi kwamba hadithi ya kisasa iko karibu na hali halisi zaidi ya maisha. Lakini haitakuwa sahihi sana kudai kuwa mandhari ya ngano, au wakati wake, havina ukweli. Kwani **ukweli** maana yake ni nini? Ukweli utategemeana na falsafa za nyakati za kazi hizo mbili za sanaa, yaani ngano na hadithi ya kisasa. Mubaalagha wa ngano usimtie upofu mhakiki akashindwa kuiona kweli iliyoubeba. Vinginevyo, ngano hutoka wapi kama si katika hali halisi ya maisha?

### 3.3.5 Kaida/sifa za hadithi fupi:

Mwisho, inaelekea kuwa mtunzi ameuchukua moja kwa moja mkabala wa kimagharibi katika kuitazama hadithi fupi ya kisasa ya (au katika) Kiswahili. Na hususan ameathiriwa vilivyo na Esenwein. Tunasema hivyo kutokana na jinsi mtunzi alivyozifikiria kaida (sifa) za hadithi fupi ya kisasa ya Kiswahili (uk. 13 - 14). Je, ni kawaida kukutana na hadithi fupi (au hata ngano) yenye mhusika mmoja tu au wawili? Je, 'kusema uwongo' katika hadithi kuna maana gani? Kwani kusema uwongo, yaani **kudanganya** na 'kutia chumvi' ni mambo mawili tofauti, la mwisho ni mbinu inayoruhusiwa katika sanaa ya uandishi. Kaida hiyo ya tatu inapingana kwa namna fulani na kaida ya nne. Kaida ya tano inadai kuwa ngano haina msuko (wa matukio). Je, hii ni kweli? Kuna hadithi gani isiyo na msuko wa matukio? **Kila hadithi** ina msuko wa matukio, iwe ngano au hadithi ya kisasa, isipokuwa kuna msuko wa matukio ulio sahili au tata, na ulio mzuri au mbaya. Kauli hiyo ya hadithi kutokuwa na msuko wa matukio ilikuwa ni maarufu baina ya watu wa magharibi dhidi ya kazi za fasihi za nchi zinazoendelea (rej. C. Larson: **The Emergence of African Fiction**: 1978:30). Kufuatana na nadharia ya E.M. Forster (Aspects of the Novel, 1927/1955:86) msingi wa msuko wa matukio uko katika mkasa wenye **kisa** (causality). Je, kuna hadithi isiyo na kisa au visa? Forster anasema hakuna. Na kaida ya mwisho haikufafanua vizuri dhana ya 'mchangamano'.

Haya ni baadhi ya masuala yaliyojitokeza katika sehemu ya nadharia.

## 4.0 Hitimisho:

**Misingi ya Hadithi Fupi** ni kazi ambayo itasaidia sana kuimarisha ufahamu wa fasihi ya Kiswahili, hususan utanzu wa hadithi fupi za kisasa. Litakuwa ni jambo la kusikitisha kama kitabu kama hiki kitakosekana katika safu ya vitabu muhimu vya kusomeshea fasihi vyuoni na katika shule za sekondari.